NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**NA. I YA 1980**

I ASSENT,

Julius K. Nyerere

*President*

*11...* JANUARY,, 1980

## Sheria ya kubadilisha baadhi ya Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, kwa madhumuni ya kuweka masharti mapya yatokanayo na kutungwa kwa Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979

[--------------------------------------------------]

SHERIA hii imetungwa na. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Pili Katika Katiba ya Nchi, ya mwaka 1980, na itaanza kutumika tarehe 12 Januari, 1980.

Mabadiliko katika Katiba

**2.** Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977 (ambayo katika ibara zifuatazo kwenye Sheria hii itatajwa kwa kifupi kama "Katiba"), yanabadilishwa kwa namna iliyoelezwa katika ibara zifuatazo za Sheria hii.

Kufuta Ibara ya 13 na ya 14 ya Katiba na kuweka nyingine badala yake

**3.** Ibara ya 13 na ya 14 ya Katiba zinafutwa na badala yake kutakuwa na ibara mpya zifuatazo:-

"Uteuzi wa Naibu Mawaziri wa kuwasaidia Mawaziri

**13.** Rais aweza kuwateua Naibu Mawaziri ambao watawasaidia Mawaziri katika utendaji wa kazi na shughuli zao.

Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri

**14.**-(1) Rais atawateuwa Mawaziri na. Naibu Mawaziri kutoka miongoni mwa Wabunge.

(2) Bila ya kujali masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (1), iwapo kutakuwa na haja ya kumteua Waziri au Naibu Waziri baada ya Bunge kuvunjwa, basi Rais aweza kumteua mtu aliyekuwa Mbunge mara tu kabla Bunge halijavurjwa.".

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)



Badiliko katika ibara. ya 15 ya Katiba

**4.** Ibara ya 15 ya Katiba inabadilishwa kwa kufuta maneno "Waziri Mdogo" na kuweka badala yake maneno "Naibu Waziri"

Badiliko katika ibara ya l6(2) ya Katiba

**5.** Ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 16 ya Katiba inabadilishwa kwa kufuta maneno "Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar" na kuweka badala yake maneno "Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar"

Badiliko katika ibara ya 17 ya Katiba

**6.** Ibara ya 17 ya Katiba inabadilishwa kwa kufuta maneno "Waziri Mdogo" na kuweka badala yake maneno "Naibu Waziri", na vile vile kwa kufuta maneno "Mawaziri Wadogo" na kuweka badala yake maneno "Naibu Mawaziri"

Kufuta aya ya (f) ya ibara ya 23 (1) na, kuweka nyingine badala yake

**7.** Ibara ya 23 ya Katiba inabadilishwa kwa kuifuta aya ya (f) ya ibara, ndogo ya (1) ya ibara hiyo na badala yake kutakuwa na aya mpya ifuatayo:-

"(f) Wabunge wasiozidi thelathini na wawili waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutoka miongoni mwa Wajumbe Wawakilishi, na kutoka nje ya Baraza hilo;"

Kufuta ibara ya 31 ya Katiba na kuweka nyingine badala yake

**8.** Ibara ya 31 ya Katiba inafutwa na badala yake kutakuwa na ibara mpya ifuatayo:-

"Wabunge waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

**31.** Mtu hataweza kuchaguliwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kuwa Mbunge kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 23 (1) (f) ya Katiba hii ila mpaka awe na sifa za uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 26 ya Katiba hii."

Mabadiliko katika sura ya Nne ya Katiba

**9.** Sura ya Nne ya Katiba inabadilishwa kwa namna ilivyoelezwa katika ibara ya 10, ya 11,ya l2 na ya l3 za Sheria hii.

Kufuta maneno ya kichwa cha habari cha Sura ya Nne na kuweka maneno mengine badala yake

**10.** Kichwa cha habari cha Sura Na Nne ya Katiba kinafutwa na badala yake kutakuwa na kichwa cha habari kipya kifuatacho:-

**"SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR, BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR''.**

Kufuta Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Nne ya Katiba na kuweka nyingine badala yake

**11.** Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Nne ya Katiba inafutwa na badala yake kutakuwa na Sehemu ya Kwanza mpya ifuatayo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)



**"SEHEMU YA KWANZA**

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR NA RAIS WA ZANZIBAR''**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na marnlaka yake

**55.**-(1) Kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar" ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii na katika ibara zifuatazo katika Sura hii ya Katiba: hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaundwa na itatekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979.

Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na madaraka yake

**56.**-(1) Kutakuwa na Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye ndiye atakuwa Rais wa Zanzibar na Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vile vile mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

(2) Katika kutekeleza madaraka yake Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi atashika na kutekeleza madaraka hayo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979.

(3) Pamoja na madaraka yake mengine yote, Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndiye atakayewateua na kuwakabidhi madaraka Mawaziri na. Naibu Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Mapinduzi

**57.**-(I) Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atachaguliwa na wananchi wa Tanzania Visiwani kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979, na kwa kufuata utaratibu utakaowekwa kwa mujibu wa Sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar inayohusu uchaguzi kwa ujumla au uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(2) Uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utafanyika kila mara litakapotokea lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika ibara ndogo ya (2) ya lbara ya 6 ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979.

(3) Wakati wa kumchagua Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ukiwadia, Kamati Maalum ya Kamati Kuu ya Chama iliyoundwa na lbara ya 63(2) ya Katiba ya Chama (kwa ajili ya kuangalia na kusimamia shughuli zote za Serikali kwa upande wa Tanzania Visiwani) itakutana na kupendekeza majina ya watu zaidi ya mmoja kutoka Tanzania Visiwani waliotimiza umri usiopungua miaka thelathini, ambao kila mmoja wao anafaa kusimama kama mtu pekee katika uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)



(4) Majina ya watu hao waliopendekezwa katika uteuzi wa mwanzo uliofanywa na Kamati Maalum kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) yatawasilishwa kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama ambayo nayo itakutana na kufanya uteuzi wa mwisho wa jina la mtu mmoja tu atakayesimama katika uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya lbara hii.

(5) Iwapo Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama itathibitisha uteuzi wa mtu mmojawapo kati ya watu zaidi ya mmoja ambao majina yao yamewasilishwa kwake kagombea kiti, mtu huyo atasimama katika uchaguzi, na wananchi watapiga kura ya kumkubali au kumkataa, na kutegemea matokeo ya kura hiyo mambo yatakuwa ifuatavyo:-

(a) ikiwa zaidi ya nusu ya wapiga kura wote wamemkubali mgombea kiti, basi mtu huyo atakuwa amechaguliwa kuwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itamtangaza kuwa amechaguliwa;

(b) ikiwa zaidi ya nusu ya wapiga kura wote wamemkataa mgombea kiti, basi mtu huyo atakuwa hakuchaguliwa kuwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na katika hali hiyo Karnati Maalum ya Kamati Kuu ya Chama itakutana tena na kupendekeza jina la mtu mwingine, na Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama hali kadhalika itakutana tena na kufanya uteuzi wa rnwisbo, kama. ilivyoelezwa katika ibara. ndogo ya (4), na hatimaye uchaguzi utafanywa kwa mujibu wa ibara. hii ndogo.

(6) Iwapo mtu ametangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwamba amechaguliwa kuwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya 5(a), basi hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake."

Kufuta na kuweka Sehemu ya pili mpya ya Sura ya Nne ya Katiba

**12.** Sehemu ya Pili ya Sura ya Nne ya Katiba, inayohusu Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, inafutwa na badala yake kutakuwa na Sehemu ya Pili mpya ifuatayo:-

## "SEHEMU YA PILI

## BARAZA LA MAPINDUZI LA ZANZIBAR

Baraza la Mapinduzi la Zanzibar na kazi zake

**58.**-(1) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar litakalokuwa na wajumbe wafuatao, wasiozidi thelathini na tano:-

(a) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

(b) Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(C) Wajumbe wengine watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa lbara ya 13(3)(c) ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)



(2) Bila ya kuyaingilia madaraka ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi litakuwa ndicho chombo kikuu cha kumshauri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya mambo yote yanayohusika na utekelezaji wa madaraka yake ya uongozi na usimamizi juu ya shughuli za Serikali ya Zanzibar na pia utekelezaji wa madaraka yake juu ya shughuli zote za Serikali kuhusu mambo yote yasiyo mambo ya Muungano, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na yale ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979.

Kuongeza Sehemu ya Tatu katika Sura ya Nne ya Katiba

**13.** Sura ya Nne ya Katiba inabadilishwa kwa kuongeza, baada ya sehemu ya Pili ya Sura hiyo, sehemu mpya ifuatayo:-

**"SEHEMU YA TATU**

**BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR**

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar na Madaraka ya kutunga Sheria za Zanzibar

**59.**-(1) Kutakuwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar la Zanzibar. Baraza la Wawakilishi litakuwa na sehemu mbili; sehemu moja itakuwa ni Wajumbe wa Baraza hilo waliochaguliwa au kuteuliwa kwa namna itakayoelezwa na masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979, na ambao watajulikana kama Wajumbe Wawakilishi; sehemu nyingine ~ a Baraza la Wawakilishi itakuwa ni Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979.

(2) Iwapo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979, au masharti ya Sheria yoyote iliyowekwa na inayotumika Zanzibar, jambo lolote lahitaji kuamuliwa au kutekelezwa na sehemu zote mbili za Baraza la Wawakilishi, basi jambo hilo halitahesabiwa kuwa limeamuliwa au limetekelezwa ipasavyo ila mpaka liwe limeamuliwa au limetekelezwa na Wajumbe Wawakilishi na vile vile Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mujibu wa madaraka yao kuhusu jambo hilo.

(3) Madaraka yote ya kutunga, Sheria katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Kazi za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar katika utaratibu wa Chama kushika hatamu za uongozi

**59A.**-(1) Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni Kamati ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama, kwa mujibu wa Ibara ya 59(12) ya Katiba ya Chama, ambayo kazi yake ni kusimamia kwa jumla utekelezaji wa siasa ya Chama inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)



(2) Pamoja na kutumia njia nyingine zakutekeleza shughuli zake kama zilivyoelezwa katika Katiba hii na katika Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar litatekeleza kazi yake iliyoelezwa katika ibara ndogo ya(l) ya ibara hii kwa njia zifuatazo:-

(a) kwa kaiuliza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maswali mbali mbali kwenye Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

(b) kwa kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wa kila mwaka wa Makadirio ya Mapato na Matumizi; na

(c) kwa kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wahitaji kuwapo Sheria"

Mabadiliko katika ibara ya 75 na ya 76 za Katiba

**14.**-(1) Ibara ya 75 ya Katiba inabadilishwa kwa kufuta ibara ndogo ya 3 na ya 4 za ibara hiyo na badala yake kutakuwa na ibara ndogo zifuatazo:-

"(3) Baada ya uchunguzi, Tume, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, itawasilisha kwa Rais au kwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kadri itakavyokuwa, maelezo ya uchunguzi uliofanywa, maoni ya Tume juu ya shauri lote na mapendekezo yake.

(4) Masharti ya ibara hii yatatumika kwa watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na wale wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watumishi na viongozi wa Chama, wajumbe na watumishi wa Tume zote za. Serikali ya, Jamhuri ya Muungano na za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, idara za Serikali hizo, mashirika ya Umma na vyombo vingi-nevyo vya Urnma, kadri itakavyoelezwa katika Sheria iliyotungwa na Bunge, lakini masharti haya hayatatumika kwa Rais wala kwa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar."

(2) lbara ya 76 ya katiba inabadilishwa kwa kufuata ibara ndogo ya 12), ya (3) na ya (4) za ibara hiyo na badala yake kutakuwa na ibara ndogo zifuatazo:-

"(2) Mtu yeyote akiteuliwa kuwa mjumbe wa Tume ya Kudumu atalazimika kuacha mara moja madaraka ya kazi ya Waziri, Naibu Waziri, madaraka yoyote katika Chama au madaraka ya aina nyingine yoyote itakayotajwa kwa ajili hiyo na Sheria iliyotungwa na Bunge.

(3) Mtu yeyote atakayeacha madaraka ya kazi ya Mjumbe wa Tume ya Kudumu aweza kuteuliwa tena, lakini, bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara ya 91 ya Katiba hii, mtu ambaye amepata kushika madaraka ya kazi ya Mjumbe wa Tume ya Kudumu kwa muda wa miaka sita mfululizo hawezi kuteuliwa tena kuwa Mjumbe mpaka upite kwanza muda wa miaka mitatu tangu alipoacha madaraka ya kazi ya Mjumbe wa Tume ya Kudumu.

.(4) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii, Mjumbe wa Tume ya Kudumu atakoma kuwa Mjumbe na ataacha madaraka ya kazi hiyo litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:-

(a) akimaliza muda wa miaka mitatu tangu alipoteuliwa: au

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)



(b) ikiwa mjumbe huyo atashika madaraka ya aina yoyote ambayo, kama asingekuwa Mjumbe wa Tume, ingemfanya asiweze kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Kudumu."

Badiliko katika ibara ya 78 ya Katiba

**15.** lbara ya 78 ya Katiba inabadilishwa kwa kufuta ibara ndogo ya (2) ya ibara hiyo na kuweka badala yake ibara ndogo ifuatayo:-

"(2) Kwa madhumuni ya ibara hii, maana ya kiongozi na masharti ya uongozi itabidi ifahamike kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Chama, masharti ya Katiba hii, masharti ya Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979, au masharti ya Sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge, kwa kadri masharti hayo yanavyohusika na suala la uongozi na ufafanuzi wake."

Mabadiliko katika ibara ya 91, ya 92 na ya 93 za Katiba

**16.** Ibara ya 91, ya 92 na ya 93 za Katiba zinabadilishwa katika ibara ndogo ya (4) ya ibara ya 9 1, ibara ndogo ya (1) na ya (3) za ibara ya 92, na katika ibara ndogo ya (1) ya ibara ya 93, kwa kufuta maneno "Waziri Mdogo", kila yanapotokea katika ibara ndogo hizo, na kuweka badala yake maneno "Naibu Waziri"

Mabadiliko katika ibara ya 94 ya Katiba

**17.** lbara ya 94 ya Katiba inabadilishwa katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hiyo.

(a) kwa kuweka, kabla ya neno "Chama" na ufafanuzi wake, maneno "Baraza la Wawakilishi la Zanzibar" na ufafanuzi wake kama ifuatavyo:-

""Baraza la Wawakilishi la Zanzibar" maana yake ni Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lililoanzishwa na Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 1979, na ambalo limetajwa katika ibara ya 59 ya Katiba hii;" ;

(b) kwa kufuta maneno "Waziri Mdogo" yaliyoko katika ufafanuzi wa neno "Waziri" na kuweka badala yake maneno "Naibu Waziri"

---

Imepitishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano tarehe 2 Januari, 1980.

..........................................
*Katibu wa Bunge*

Nathibitisha kwamba Muswada kwa ajili ya Sheria hii umepitishwa na Bunge lewa mujibu wa masharti ya ibara 52)(1) (a) ya Katiba.

..........................................
*Spika*

Imepigwa Chapa - Mpigachapa wa Selikali, Dar es Salaam, Tanzania.